

Happy New Year! Don't Be A Hypocrite

January 5, 2020

Matthew 23:25-39

I. Happy New Year!

- A. Why talk about this?!
- B. What is hypocrisy? (Matthew 6:1, 3, 16)

II. Cups and Tombs

- A. It's a lemon
- B. Dirty dishes (Luke 11:39-41)
- C. Whitewashed tombs (Romans 6:19)

III. A History of Violence

- A. Speaking of tombs ...
- B. Your fathers' children
- C. The measure of your fathers (Luke 11:49)

IV. Judgment on Jerusalem

- A. Blood that speaks (Matthew 10:4; Genesis 4:10; 2 Chronicles 24:20-22)
- B. The house left desolate (Malachi 3:1; John 1:11; Hebrews 13:2; Philippians 2:11)
- C. The compassionate Lord (2 Samuel 19:4; Psalm 36:7; 91:4; Ruth 2:12)
- D. A better word (Hebrews 11:28; 12:18-24; Isaiah 40:1-2)

Mathayo 23:25-39

25 Ole wenu waandishi na Mafarisayo, wanafiki! Kwa kuwa mnasafisha nje ya kikombe na chano, na ndani yake vimejaa unyang'anyi na kutokuwa na kiasi. *26* Ewe Farisayo kipofu, safisha kwanza ndani ya kikombe, ili nje yake nayo ipate kuwa safi. *27* Ole wenu, waandishi na Mafarisayo, wanafiki! Kwa kuwa mmeefanana na makaburi yaliyopakwa chokaa, nayo kwa nje yaonekana kuwa mazuri, bali ndani yamejaa mifupa ya wafu, na uchafu wote. *28* Vivyo hivyo ninyi nanyi, kwa nje mwaonekana na watu kuwa wenye haki, bali ndani mmejaa unafiki na maasi. *29* Ole wenu, waandishi na Mafarisayo, wanafiki! Kwa kuwa mnayajenga makaburi ya manabii, na kuyapamba maziara ya wenye haki, *30* na kusema, Kama sisi tungalikuwako zamani za baba zetu, hatungalishirikiana nao katika damu ya manabii. *31* Hivi mwajishuhudia wenyewe, ya kwamba ninyi ni wana wao waliowaua manabii. *32* Kijazeni basi kipimo cha baba zenu. *33* Enyi nyoka, wana wa majoka, mtaikimbiaje hukumu ya jehanum? *34* Kwa sababu hiyo, angalieni, mimi natuma kwenu manabii na wenye hekima na waandishi; na wengine wao ninyi mtawaua na kuwasulibisha, na wengine wao mtawapiga katika masinagogi yenu, na kuwafukuza mji kwa mji; *35* hivyo ije juu yenu damu yote ya haki iliyomwagika juu ya nchi, tangu damu ya Hibili, yule mwenye haki, hata damu ya Zakaria bin Barakia, mliyemwua kati ya patakatifu na madhabahu. *36* Amin, nawaambieni, Mambo hayo yote yatakuja juu ya kizazi hiki. *37* Ee Yerusalem, Yerusalem, uwauaye manabii, na kuwapiga kwa mawe wale waliotumwa kwako! Ni mara ngapi nimetaka kuwakusanya pamoja watoto wako, kama vile kuku avikusanyavyo pamoja vifaranga vyake chini ya mabawa yake, lakini hamkutaka! *38* Angalieni, nyumba yenu mmeachiwa hali ya ukiwa. *39* Kwa maana nawaambia, Hamtaniona kamwe tangu sasa, hata mtakaposema, Amebarikiwa ajaye kwa jina la Bwana.